

## **LBE 2009 – Migration**

### **Episode 5:**

### **Students in Germany**

**Author:** Florent Kossivi Tiassou

**Editor:** Thomas Mösch

**Translator:** Anne Thomas

#### **Characters:**

**Narrator**, male

***Inserts (French):***

**Muriel**, young woman

**Améle**, young woman (1 insert only)

#### **Intro:**

Hujambo na karibu kwenye sehemu nyingine katika makala ya Noa Bongo Jenga Maisha yako kuhusu Uhamiaji kati ya Afrika na Ulaya. Leo tunakutana na Muriel, msichana kutoka Cameroon ambaye alikuja hapa Ujerumani kwa ajili ya kuendelea na elimu ya chuo kikuu.

---

<b>1. Atmo conversation</b>
-----------------------------

#### **2. Narrator:**

Akiwa na digirii yake ya uzamili yaani Masters Degree, Muriel alifika hapa Ujerumani mnamo Januari mwaka 2006 kwa ajili ya kuendelea na masomo yake ya uchumi na Biashara. Mara tu alipofika alikumbana na maisha ya wanafunzi katika nchi ya kigeni.

Licha ya yote yanayotokea katika maisha yake , msichana huyu mwanafunzi mwenye miaka 25-kutoka Cameroon alikuwa kama mwehu pale tulipomuuliza kuhusu siku zake za mwanzoni hapa nchini Ujerumani tangu miaka miwili iliyopita.

### **3. O-Ton Muriel (French)**

**Nilishangaa kweli kwa mara ya kwanza nilipoona theluji. Ilikuwa kama vile mbingu katika ardhi. Ilipendeza sana. Kwa bahati mbaya nilikuwa sehemu ambayo theluji ilianguka kwa wingi mpaka miezi mitatu baadaye nikaichukia.**

### **4. Narrator:**

Alikaribishwa na baridi kali, Muriel hakuwa amejitayarisha vyema kukabiliana na hali halisi. Msichana huyo kutoka Cameroon kwanza aliishi katika nyumba za wanafunzi katika mji wa Essen, eneo la Ruhr lililo katikati ya jimbo la viwanda magharibi mwa Ujerumani. Ukubwa wa chumba chake ulikuwa nusu ya chumba chake cha nyumbani Cameroon. Lakini hilo halikuwa tatizo na baada ya miezi sita alifaulu mtihani wake wa kwanza – na huo ulikuwa ni mtihani wa lugha. Hapo, alidhani kuwa ataweza kuanza masomo yake ya Uchumi na Biashara katika chuo kikuu cha Essen-Duisburg. Lakini kumbe alikuwa akisuburiwa na maajabu mengine. Lugha yake ilikuwa bado hafifu na isitoshe shahada yake kutoka Afrika ilikuwa vigumu kukubalika kwa sababu alifahamishwa kuwa viwango vilikuwa duni. Chuo kikuu kilikataa kumuweka Muriel katika kozi ya shahada ya uzamili. Anapozungumza kuhusu siku zake za mwanzoni katika chuo kikuu, tabasamu yake yote inatoweka.

### **5. O- Ton Muriel (French)**

**Ilinibidi nifanye tena kozi ya shahada ya kwanza na baadae nikafanya mitihani. Nilitumia mihula mitatu au minne kufanikisha hilo. Kwa ufupi nilirudia kufanya digrii yangu ya kwanza ambayo tayari nilikuwa nayo na pia nilikuwa na shahada ya uzamili yaani master's.**

#### **6. Narrator:**

Mwishowe msichana huyo mwanafunzi alipata nafasi ya kusomea digrii ya uzamili katika chuo kikuu cha Bochum, mji ambao hauko mbali na mji wa Essen.

#### **7. O-Ton Muriel (French)**

**Kitu ambacho hata chuo nilichosomea wasingeweza kunipa! Ni kama vile walijaribu kunirudisha nyuma, tena kwenye kiwango cha chini.**

#### **8. Narrator:**

Lakini japo kweli alipata nafasi huko Bochum, lakini hilo halikuwa suluhisho la matatizo yake yote. Hapa Ujerumani, kwa sasa lazima ulipe karo kwa masomo ya chuo kikuu. Muriel hapati msaada wowote kutoka nchini mwake tofauti na wanafunzi wa Kijerumani ambao mara nyingine hupata msaada kutoka serikalini unaojulikana kama Bafög. Inamlazimu Muriel kujilipia karo yake yeye mwenyewe.

#### **9. O- Ton Muriel (French) *(if you need to shorten the script, cut this insert out)***

**Mara nyingine mimi hukosa masomo kwa ajili ya kufanya kazi, ingawa sifanyi hivyo wakati wa mitihani, tuko Ujerumani hapa kila kitu kiko kwenye mpangilio, mwanafunzi hawezi kufukuzwa**

**kwenye nyumba kwa sababu hajalipa kodi. Mara nyingine mimi huchelewa kulipa kodi yangu lakini sijali kwa kuwa nina lengo ambalo nataka kulitimiza.**

**10. Narrator:**

Lakini kuna shida pia nchini Ujerumani wanafunzi wa kigeni hawaruhusiwi kufanya kazi zaidi ya siku 90 kwa mwaka. Lakini Muriel hataki jingine lolote ila kumaliza digrii yake ya uzamili hapa Ujerumani. Anakumbuka shida zinazowafika wanafunzi katika nchi yake. Na hii inaeleza wazi kwa nini nchi za Ulaya hazikubali kwa urahisi matokeo ya masomo kutoka nchi za Kiafrika.

**11. O-Ton Muriel (French)**

**Nilikuja hapa kwa kuwa nilidhani kwamba elimu ya Ulaya ni bora kuliko ile tunayopata nyumbani. Chuo nilichosoma zamani, kwa mfano – tulikuwa karibu wanafunzi 2,000 katika kitivo cha menejimenti na ukumbi ulikuwa na takriban nafasi 700. Kwa hivyo mtu alilazimika kufika pale mapema ili kuwahi nafasi ya kukaa, ukichelewa basi hupati kiti. Wakufunzi wetu kila mara wanasafiri kuja Ulaya na hiyo inamaana kuwa hakuna masomo. Mfumo wa elimu ya chuo kikuu wa hapa umepangwa barabara kuliko kwetu. Nyumbani tunasoma tu bila kujua malengo ya usoni. Hapa Ulaya swali ni, je. Nitasomea utaalamu wa somo gani?"**

**12. Atmo – keyboard / [aus Archiv](#)**

**13. Narrator:**

Katika chuo kikuu cha Essen-Duisburg, Muriel amesomea utalaamu katika somo la fedha. Wanafunzi wanapata mahitaji yote ili kuwarahisishia kazi zao. Muriel anatumia muda mwingi katika maktaba ya chuo kikuu. Kuna sehemu ya IT ambapo wanafunzi wanaweza kufanya utafiti wao vizuri na kwa urahisi. Sivyo ilivyo nchini Cameroon:

#### **14. Atmo+voice clip Muriel (French)**

***(at the library)***

**..... kama unavyoona, hii ni maktaba ya kompyuta, nikigonga hapa ninapata fursa ya kuingia kwenye vitabu vyote. Kila mwanafunzi anaelipa karo anaweza kuchukua vitabu kutoka hapa.**

***(sound of books)***

#### **15. Narrator:**

Sehemu anayo fanyia kazi Muriel haiko mbali. Hivi karibuni alipata kazi kwenye chuo kikuu ambako anafanya kwa muda wa saa mbili mara tatu kwa wiki. Mapato anayopata, yanamsaidia kulipia masomo yake na pia kuwatumia jamaa zake fedha kidogo:

#### **16. O-Ton Muriel (French)**

**Kupata kazi hii, ilinibidi kusoma sana, na kufanya utafiti kwenye internet. Mpaka uangalie ili kupata... *(Atmo her phone rings)***

**Ah! Subiri kidogo tafadhali... nina simu. Yes, hello? (...) Hello**

**mama, ndio sijambo. , nzuri tu. (...) Wow – Nashukuru kwa**

**kunikumbuka jioni hii. (...) Hata ndio kwanza nimerudi,**

**nimechoka. *(Continues in one of the languages of Cameroon)*...**

**(...)**

**(Continues in French) :**

**...Ndio!. Alikuwa mama yangu aliyenipigia. Alitaka kujua hali yangu. Tulikuwa hatujazungumza kwa siku chache na ndugu zetu kule Afrika huwa wana wasiwasi. Wanapiga kila baada ya siku mbili au tatu kujua mambo yanaendeleaje. Ameniuliza kama ninahitaji msaada , ameniambia nimpigie iwapo ninataka msaada. Maskini mwanamke wa watu, siwezi kumweleza kuhusu kila kitu cha huku. Wanaponipigia simu mimi hufurahi sana, sijisikii upweke, ninajiona kama niko pamoja na familia yangu.**

### **17. Narrator:**

Wazazi wa Muriel pamoja na familia yake wako Cameroon, lakini msichana huyo anasema kuwa ameanza kujisikia yuko nyumbani hapa nchini Ujerumani. Ana mawasiliano mazuri chuoni na katika dahalia la wanafunzi. Ni mawasiliano ambayo yamemuwezesha kujumuika vyema na jamii:

### **18.O-Ton Muriel (French)**

**Ni muhimu sana kuwa na marafiki wa Kijerumani sio tu kuzungumza kwa ajili ya kupata mazoezi ya kuendeleza lugha, lakini hata wao wapate fursa ya kutufahamu . Wanafahamu vyema mambo ya hapa chuoni na kwa hiyo wanatusaidia. Mara nyingine hatuelewi kitu basi wao wanatusaidia. Rafiki zetu wa Kijerumani wanatueleza maana ya mambo mengi ambayo hatuyaelewi.**

### **19. Music (free choice)-----**

## **20. Narrator:**

Hii ni mara yetu ya pili kukutana na Muriel, miaka miwili baadae.

Kila kitu kinamwendea vyema:

## **21. O-Ton Muriel (French)**

**Ninaendelea na masomo yangu vizuri. Nipo katika awamu ya mwisho ya shahada yangu ya uzamili yaani 'Master's' na hivi sasa naandika tasnifu yangu yaani 'dissertation'. Haikuwa rahisi hapo mwanzoni.**

## **22. Narrator:**

Kuna wanafunzi wengi ambao hushindwa kuvumilia na hatimae kuacha masomo yao wakati mwingine Muriel huzongwa na mawazo kama hayo. Wengine wao hugeuka kuwa wahamiaji wasio halali na wengine hurudi kwao. Kila mwanafunzi katika dahalia la akina Muriel ana hadithi yake ya kueleza. Amélé ni msichana wa Kinaigeria-na Kitogo. Ni jirani yake Muriel na ameishi hapo kwa muda mrefu zaidi:

## **23.O-Ton Amélé (French.)**

**Tulikutana hapa kwenye dahalia (Hostel) letu la wanafunzi. Alinielezea matatizo yake. Na mimi nilifahamu kuwa huyu ni mwanamke anaejua kupigania maisha yake. Alifanya kazi Düsseldorf. Ungeweza tu kutambua kwamba alikuwa na ari ya mafanikio. Alikuwa tayari kufanya kazi yoyote kwa ajili ya kulipa karo yake. Wageni wote wana shida za kufanana. Hata mimi nilipitia hayo. Mara nyingi inakuwa mifumo ya elimu haiko sawa**

**au hawakubali kutambua kiwango chetu na kwa hivyo wanaturudisha nyuma.**

#### **24. Music (free choice)-----**

##### **25. Narrator:**

Muriel alitaka kurudi Cameroon siku chache tu baada ya kufika hapa Ujerumani:

##### **26. O-Ton Muriel (French)**

**Mwanzoni nilitaka kurudi, kwa sababu nilivunjika moyo, lakini sasa nimejumuika vyema na jamii, sina tena mawazo hayo ya kutaka kurudi. Ninataka kutimiza lengo langu kabla ya kurudi nyumbani, bila ya hivyo nitakuwa napeleka nini nyumbani kutoka Ulaya?**

##### **27. Narrator:**

Kitu kimoja kinachomuweka Muriel karibu na nyumbani licha ya kuwa haishi huko kwa sasa ni chakula. Hataki kabisa kubadili mfumo wake wa kula chakula cha Kikameron kwa Soseji za Kijerumani.

##### **28. Atmo Kitchen / [aus Archiv](#)**

##### **29. Narrator:**

Kwenye jiko lake dogo lililo mlangoni tu ukiingia kwenye nyumba yake ndogo, kuna mboga za Kiafrika. Zinaweza kuwa ghali lakini anazinunua kuongezea mlo tofauti kwenye maankuli yake:

##### **30. O-Ton Muriel (French)**



**Kama unavyoona, ule pale ni wali na mchuzi. Wakati wa chakula cha mchana, nakula chakula cha Kijerumani na jioni nakula chakula cha Kiafrika. Ninapenda hivyo. Mazoea yana Tabu!**

**31. Narrator:**

Anatamani nyumbani, anaweka muziki – Makossa - ni mtindo wa muziki wa Kikameroon:

**32. Atmo (Music+voice clip (Muriel, French.) :**

**Kusema kweli niatamani kama ningeweza kwenda nyumbani japo kwa usiku mmoja halafu nikarudi kesho.**

***Music up***

**Outro:**

Na mpaka hapo ndio tumekamilisha kipindi chetu kwa leo. Makala hii imeandikwa na Florent Kossivi Tiassou. Kumbuka unaweza kusikiliza vipindi vyote vya Noa Bongo Jenga Maisha Yako kutoka Deutsche Welle kwenye mtandao anuani yetu ni: [www.dw-world.de/lbe](http://www.dw-world.de/lbe)

Usisahau kujiunga nasi tena katika makala ijayo. Hadi hapo. Kwaheri.

----(End)----